HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA

# JARIDA MAALUM

## Maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano

*"Umoja na Mshikamano ndiyo nguzo ya kukuza Uchumi wetu"*



# RC MTWARA ASISTIZA UMOJA NA MSHIKAMANO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe.Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesisitiza umoja na mshikamano katika kutekeleza majukumu mbalimbali ngazi ya Mkoa ili kuunganisha nguvu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu

Amesema hayo Aprili 26,2023 katika kilele cha maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambapo Kimkoa yamefanyika katika kijiji cha mchichira Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ambayo yana kauli mbiu inayosema "Umoja na Mshikamano ndiyo nguzo ya kukuza Uchumi wetu "

Aidha Mkuu wa Mkoa amekabidhi zawadi kwa washindi mbalimbali walioshinda katika mashindano ya insha,timu za mpira,watoa burudani na skauti katika maadhimisho hayo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg. Mussa Gama akisoma taarifa yake ameipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya Maendelea ambapo imeboresha huduma ya afya,maji, elimu na barabara katika Halmashauri ya Tandahimba.






# RC AKABIDHI MAGARII KWA WAKUU WA WILAYA YA TANDAHIMBA NA NEWALA





Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed amekabidhi magari mawili na kusisitiza magari hayo yakaboreshe ujifunzaji na ufundishaji ili kuleta mabadiliko ya elimu katika mkoa.

Magari hayo yalitolewa na Serikali Kuu Aprili 20,2023 ,ameyakabidhi aprili 26,2023 kwa Wakuu wa Wilaya ya Tandahimba na Newala ambao nao wameyakabidhi kwa Wakurugenzi wa Halmashauri hizo ambapo wametakiwa kuyatumia kama ilivyokusudiwa.

Aidha Mkuu wa Mkoa wa Mtwara akiwa kijiji cha Mchichira katika sherehe za maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano amezindua nyumba na ofisi ya Afisa Tarafa Mchichira.

Katika kilele cha maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wananchi walipata huduma za kupima Malaria, Ukimwi, BP, kuchangia damu, kupima uzito, chanjo ya Covid-19, utoaji wa chanjo kwa watoto na huduma za lishe ambazo zilitolewa kati eneo hilo.



# DC SAWALA AONGOZA WANANCHI UJAZAJI KIFUSI MRADI WA UJENZI SHULE SHIKIZI MNARANI

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mhe. Kanali Patrick Sawala akiwa pamoja na Kamati ya Usalama Wilaya (KU) na Timu ya Menejimenti (CMT) walishiriki kuweka kifusi katika mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi moja ya walimu shule shikizi Mnarani kata ya Mchichira kuunga jitihada za miradi ya maendeleo

Akizungumza na wananchi waliojitokeza kwa wingi kushiriki katika uwekaji wa kifusi Aprili 25,2023 Dc Sawala aliwapongeza wananchi kwa kuibua miradi ya Maendeleo ambapo amesema juhudi hizo ziendelee ili kukamilisha mradi huo wanafunzi waanze kusoma katika shule hiyo.

Aidha alitumia nafasi hiyo kuwasisistiza wananchi kuhuisha taarifa za mikorosho yao katika zoezi la uhuishaji wa kanzi data za wakulima ili kupata takwimu sahihi ambayo itasaidia wakati wa ugawaji wa pembejeo.





## MKURUGENZI GAMA AONGOZA MDAHALO WA MIAKA 59 YA MUUNGANO

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Mussa Gama Aprili 25,2023 ameongoza mdahalo katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri

Katika mdahalo huo washiriki walitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu tulipotoka tulipo na tunapoelekea ambapo walisistiza kuendelea kuunganisha Umoja na Amani ili kuenzi Muungano ambao umetimiza miaka 59

Aidha walishauri Serikali kuendelea kutoa ajira kwa vijana ,kuenzi kundi la wazee hasa katika upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee sambamba na historia ya Muungano itolewe mashuleni kuuenzi









## TIMU YA TANDAHIMBA HQ YAICHAPA MCHICHIRA COMBINE BAO 1-0



Timu ya mpira wa Mguu ya Tandahimba HQ imeiibuka mshindi dhidi ya timu ya Mchichira Combine kwa kuichapa bao 1-0 katika mechi iliyofanyika Aprili 25,3023 katika uwanja wa Mpira wa Mchichira

Timu ya Tandahimba HQ ikiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Mhe. Baisa Baisa waliibuka kidedea na kushinda zawadi ya Mbuzi katika mechi hiyo

Mechi hizi zimefanyika kuamsha ari kwa wananchi katika kusherekea maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo Kimkoa yamefanyika katika kijiji cha Mchichira Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.


## MADARASA MAWILI YA AWALI YA MFANO YAZINDULIWA MJIMPYA

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed amezindua mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali ya mfano yenye thamani ya shilingi milioni hamsini na tano laki nane na elfu arobaini( 55,840,000 ) katiia shule ya msingi Mjimpya iliyopo kata ya Tandahimba

Uzinduzi huo umefanyika Aprili 26,2023 ambapo ni miongoni mwa shughuli zilizofanyika katika kilele cha maadhimidho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo Kimkoa yamefanyika kijiji cha Mchichira Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba

Mradi huo ambao umeambatana na ununuzi wa michezo ya watoto umeboresha mazingira ya wanafunzi hususan wa darasa la awali.







# WANANCHI WA MCHICHIRA WASHIRIKI KUFANYA USAFI WA MAZINGIRA





Katika kuadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Wananchi wa Kata ya Mchichira Aprili 24,2023 walishiriki kufanya usafi wa mazingira katika makazi yao sambamba na ofisi ya tarafa,kituo cha afya na shule shikizi

Akizungumza na wananchi wa mchichira katika ofisi ya tarafa ya mchichira Katibu Tawala Wilaya ya Tandahimba Ndg. Juvenile Mwambi aliwapongeza wananchi kwa kushiriki kuweka mazingira yanayowazunguka safi


Naye Diwani wa Kata ya Mchichira Mhe.Jamali Mtonya alisema kwamba wananchi wa Mchichira wapo tayari kwa ajili ya maadhimisho ya Muungano Kimkoa.

## WAZEE WAIPONGEZA SERIKALI KUIMARISHA MUUNGANO

Wazee Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba wameipongeza Serikali kwa kuendelea kuulinda na kuuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

Wakizungumza kwa nyakati tofauti Aprili 24 katika mahojiano maalum wamesistiza kuwa ili kuendelea kuuenzi Muungano Elimu itolewe kwa wanafunzi mashuleni ili waweze kujua historia ya Muungano na kuendelea kuuenzi.


























Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba